

SPISHI ZA MIMEA VAMIZI ISIYO YA ASILI TANZANIA: NI ZIPI?

Esther F. MVUNGI

Idara ya Elimu Mimea, Chuo Kikuu Dar es Salaam, S.L.P 35060, Dar es Salaam, Tanzania

SPISHI YA MIMEA VAMIZI ISIYO YA ASILI NI NINI?

Spishi ya mimea Vamizi usiyo asili ni mimea ambao kwa makusudi au kwa bahati mbaya uliingizwa nje ya mazingira yake ya asili ukasitawi na kuanza kuzaliana. Mara nyingi mimea vamizi isiyo ya asili inasambaa kwa kasi katika maeneo yake mapya ikimiliki rasilimali-mwanga, virutubisho, maji, nafasi, nakadhalika na kusababisha madhara kwa spishi zingine haswa za asili

SIFA ZA MIMEA VAMIZI ISIYO YA ASILI

- ◆ Uwezo mkubwa wa kushindana
- ◆ Kukua haraka na /au kiwango cha uotaji mbegu kikubwa
- ◆ Uwezo mkubwa wa kuzalisha mbegu au vipandikizi
- ◆ Hitaji la kukua kila eneo



HALI YA MIMEA VAMIZI ISIYO ASILI TANZANIA


- Zaidi ya mimea 10 vamizi isiyo asili inajulikana, mf.:
- ◆ *Cedrela odorata* katika Msitu wa Hifadhi Kimboza
 - ◆ *Maesopsis eminii* kwa wingi Usambara Mashariki
 - ◆ *Lantana camara*
 - ◆ *Mimosa pigra*
 - ◆ *Clidemia hirta*
 - ◆ *Psidium cattleianum*
 - ◆ *Landolphia owariensis*
 - ◆ *Phyllostachys bambusoides*
 - ◆ *Castilla elastica* (Raba ya Panama)
 - ◆ *Acacia mearnsii*
 - ◆ *Opuntia* sp.
 - ◆ *Eichornia crassipes*, n.k.

JINSI GANI MIMEA ISIYO ASILI INAVYOINGIZWA?

MAMBO YANAYOCHANGIA MIMEA ISIYO ASILI KUVAMIA

- ◆ Shughuli za kuhifadhi kwa kukagua, Kuzuia upepo au mmomonyoko wa ardhi, n.k
- ◆ Kuingizwa kwa bahati mbaya kupitia uchafuzi wa vitu vinavyoingizwa mf. *Clidemia hirta*
- ◆ Kutoka kwa bahati mbaya kwenye taka za kilimo zilizotupwa mf. *Mimosa pigra*
- ◆ Kupanda kwa makusudi katika mfumo wa uotaji asili usiodhibitiwa, kuzuia mmomonyoko wa ardhi, usawazishaji wa ardhi, n.k., mf. *Lantana camara*, *cedrela odorata*, n.k
- ◆ Kuendelea kukua katoka mifumo ya kilimo inayodhibitiwa mf. *Psidium cattleianum*

Hatua za uvamizi



Mambo yanayotokana na spishi

- ◆ Maingiliano / Ushindani
- ◆ Nasaba yake
- ◆ Kuwezesha

Mambo yanayoambatana na Ikolojia

- ◆ Rasilimali zisizotumika
- ◆ Nafasi zisizojazwa / uwazi
- ◆ Mfumo wa ikolojia usio dhabiti
- ◆ Usimamizi wa ardhi

KWA NINI MIMEA VAMIZI ISIYO ASILI INAFANIKIWA?

- ◆ Katika mazingira yake mapya, inakosa maadui wa asili na magonjwa kudhibiti ukuaji au kuzuia kuzaliana kwa mafanikio
- ◆ Ina njia nzuri za kutawanya mbegu mf.inatoa mbegu zenye maji ya usukari yanayovutia ndege na wanyama wengine au zinatawanywa na upepo hivyo kuchukua umbali mkubwa
- ◆ Baadhi, ina mifumo ya mizizi inayosambaa na kuathiri mifumo ya mimea mingine inayoizunguka
- ◆ Baadhi inatoa kemikali katika majani yao au mifumo ya mizizi inayoziua ukuaji wa mimea mingine inayoizunguka
- ◆ Mingi kati yao hustawi kwenye udongo uliotibuliwa, kama vile kwenye maeneo mapya yanayoendelezwa



NI NINI MIMEA ISIYO ASILI INACHOFANYA KWENYE MFUMO ASILI WA IKOLOJIA?

- ◆ Inashindana moja kwa moja na spishi asilia kwa rasilimali: mwanga, maji, virutubisho, n.k
- ◆ Inabadilisha uhusiano wa ki-ikolojia miongoni mwa spishi asilia na kuathiri ufanyaji kazi mifumo ya Ikolojia, manufaa ya mifumo na afya ya binadamu
- ◆ Kwenye kiwango kikubwa, inaweza hasa kupunguza aina na idadi ya mimea asilia, hivyo kuathiri mfumo wa chakula, sehemu za maficho na sehemu wanakozaliana wanyama
- ◆ Inaweza kupunguza kumiminika kwa vijito na kupunguza kiwango cha maji ya chini
- ◆ Kwa ujumla, inaweza kubadilisha michakato ya kawaida ya Ikolojia na mahusiano yanayosaidia mimea asilia na wanyama katika eneo, mf. kutowesha mimea muhimu ya malazi au wanayotoa chakula kwa ndege

TUNAWEZA KUFANYA CHOCHOTE KUHUDU SPISHI ZA MIMEA VAMIZI ISIYO ASILI?

- ◆ Zuia kuongeza, kuingiza uwezekano wa mimea vamizi isiyo asili
- ◆ Panda miti asili pekee kuziba nafasi kuepuka mimea vamizi kuota
- ◆ Ongeza juhudi za kudhibiti spishi za mimea vamizi isiyo asili, zuia kusambaa kwao, na zuia kusitawi na kuanzisha mimea mingine
- ◆ Weka sheria kali inayopiga marufuku kupanda mimea vamizi isiyo asili katika eneo fulani mf. vyanzo vya maji
- ◆ Jifunze na kutambua hatari na madhara ya mimea vamizi isiyo asili
- ◆ Tumia njia za kung'oa, kemikali na kibalugia kuzuia mimea isiyo ya asili